**Learning by Ear**

**People Who Make a Difference**

David Kimaro,

Orphanage: Living-Water-Children-Center, Arusha/Tanzania

Author: Friederike Eversheim, Communication & Consulting, Krefeld
Editor: Stefanie Duckstein, Tony Dunham

Sound clips in DALET: Learning by Ear: PEO_Kimaro_xxx (Bis inklusive O-Ton 17 geschnitten)

CHARACTERS:

**Narrator:** (female)

**O-Tones**

- O-Tone 1: David Kimaro, 26
- O-Tone 2: Dorah Kimaro, Mother, ca. 50
- O-Tone 3: Anza Kimaro, Father, ca. 50
- O-Tone 4: Child from Orphanage, ca. 6

**Introduction (Announcer):**

Hujambo msikilizaji wa Noa Bongo Jenga Maisha Yako. Katika makala haya ya Watu wanaoleta Mabadiliko unapata fursa ya kuwajua mashujaa katika maisha ya kila siku barani Afrika. Watu hao ni mashujaa, hawababaishwi na panda shuka za maisha ya kila siku kwa sababu wana ndoto ya maisha ya baadaye. Leo hii tunakwenda huko kaskazini mwa Tanzania katika mji wa Arusha ambako tutakutana na kijana David ambaye ana familia kubwa si haba

**TEXT:**

1. **ATMO:** Children singing and walking around
   (Track 1007, 0.03, FADE INTO NARRATOR)

2. **NARRATOR**
   Hamjambo, hebu fikiria iwapo kama unaweza kuishi na ndugu 50 wa kike na wa kiume kwenye familia moja? Najua unafikiria kuwa hiyo haiwezekani kabisa, lakini inawezekana, tunamfahamu mtu anayeishi na familia kubwa kabisa, jina lake ni David Kimaro ana umri wa miaka 26. Wazazi wake wana nyumba ya kuwatunza watoto yatima katika mji wa Arusha nchini Tanzania, makao hayo ya watoto yatima yanaitwa The Living Water Children Center. Cha kushangaza ni kwamba David hakasiriki wala hachoshwi na kelele na mahitaji mengi ya watoto hao.

3. **ATMO**: “Hamjambo wageni wetu!” (Track 1006, 0.16-0.22, FADE INTO NEXT ATMO)

4. **ATMO**: Noise of children in the Living-Water-Children-Center (Track 1009, 0.40-0.43)

5. **NARRATOR**

   Takriban watoto 30 wamesimama mbele ya nyumba ndogo nyeupe ambayo inaonekana tu kama nyumba ya kawaida ya mjini. Nyumba hiyo ipo mwisho wa barabara kwenye kona. Wageni lazima wapite kwenye lango la chuma ambalo limechorwa kwa picha za wanyama, picha hizo zimechorwa na watoto hao. David alikuwa bado katika shule ya upili wakati wazazi wake walipomchukua mtoto wa kwanza kumlea miaka michache iliyopita. Bila shaka alishtuka alipofika nyumbani, au ilikuwaje?

6. **OTONE David:** (Track 1029, English, 0.10-0.50) (Track 1030, Swahili)

   ”Nilirudi nyumbani baada ya kuishi miaka mingi Nairobi ambako nilikuwa nasoma. Na wakati huo mama yangu alikuwa na wazo la kuleta watoto nyumbani kwetu. Nilifurahi sana kwa sababu nilifahamu kuwa lilikuwa ni wazo zuri kuwaleta watoto katika familia, yaani watoto masikini au watoto walemavu ambao huwa tunawaona barabarani, ili nao wapate fursa ya kuwa nyumbani, wawe angalau na paa juu yao na mtu wa kuwaangalia.”

7. **NARRATOR**:

Na mtu huyo wa kuwaangalia si mwingine bali ni David mwenyewe. Miaka michache iliyopita aliamua kusimamia makao hayo ya watoto yatima. Lakini kuangalia au kucheza na watoto hao tu hakutoshi. Usimamizi kabambe unahitajika. David amehitimu chuo kikuu, ana shahada ya usimamizi kutoka chuo kikuu na hicho ndicho alichokihitaji ili kukabiliana na shida mbali mbali za kila siku katika usimamizi wa makao hayo.

8. **OTONE David:** (Track 1072 English, 0.14 – 0.30) (Track 1071 Swahili) (START HIGH; LATER FADE UNDER NARRATOR)

*" Hujambo mwalimu mkuu, habari za asubuhi huyu ni David, U hali gani? Mimi ni mzima, asante. Ninauliza kama ulipokea orodha ya watoto waliochelewa jana...."*

9. **NARRATOR:**

Badala ya kuendeleza kazi yake ya usimamizi katika sekta binafsi au sekta ya serikali, David ameamua kuwa mwalimu, meneja na pia baba, tena wa watoto 50.

10. **OTONE David:** (Track 1072 English, 0.46 – 0.56) (Track 1071 Swahili) *(continued talk at the phone - high)*
*"Oh, ndio, unaweza, unaweza kuniachia memo juu ya meza yangu , nitaichukua...."*

11. **NARRATOR:**
Hivi majuzi tu David alikabidhiwa mtoto mmoja mdogo aliyetelekezwa, mama wa mtoto huyo ana umri wa miaka 14 tu. David aliamua kumpa mtoto huyo nafasi ya kuishi maisha ya kawaida.

12. **OTONE David:** (Track 1044 English 0.40 - 1.08 min, Track 1045, Swahili)
*"Maisha ni magumu na yanazidi kuwa magumu kwa sababu kila kukicha watu wanapoteza kazi zao.….kila siku zinavyozidi kusonga mbele watu nao wanazidi kuwa wachoyo, wanakuwa na tamaa na kile walichonacho….kichache walicho nacho hawataki kukigawa eti kwa sababu ni kidogo. Ni vigumu sana kuwashawishi watu kama hao kujiunga nawe katika juhudi za kuwasaidia watu wengine.… Hiyo imekuwa ni changamoto kubwa inayonikabili kufanikisha hilo katika maisha ya kila siku."*

13. **NARRATOR:**

Ukifikiria maisha ya usoni – unaona umuhimu wa elimu fursa ya kwenda shule ni jambo muhimu sana hasa kwa watoto yatima. Hilo ni hakikisho la kwamba wataweza kujitafutia kazi na hata kujikimu kimaisha katika maisha yao ya baadaye. Ndani ya darasa dogo David amesimama mbele ya wanafunzi wake 20, anawafundisha herufi. Mmoja baada ya mwingine anakuja mbele ubaoni na kuandika herufi moja moja kwa chaki.

**14. Atmo: (Track 1017 English, 2.43 -2.55)**

*(David teaching: spelling, children come to the board and write the words on the board – "the word amazing".*

15. **NARRATOR:**

Mama yake David Dorah na baba yake Anza wanaukumbuka vyema utoto wa mwana wao wa kiume David.

16. **OTONE Mother**: (Track 1060 English, 0.29 - 0.42 min)

(Track 1059 Swahili)

*"Kipawa chake kilianzia utotoni alipokuwa shuleni.… aliwasaidia watoto waliokuwa na shida. Na hapo tulijua kuwa yeye ni mtoto mwenye roho nzuri. Alipokuja nyumbani*

*wakati ambapo tuliamua kuanza kuwasaidia watoto yatima yeye alikuwa mstari wa mbele kuwasaidia watoto hao waliokuwa na shida.*

17. **NARRATOR:**

Mchango mkubwa wa mtoto wao umewatia moyo bwana Anza na mkewe Dorah Kimaro wa kupanua makao hayo ya watoto. Wamenunua kiwanja katika sehemu iliyo kilomita 15 kutoka mjini Arusha na mwaka jana walianza ujenzi wa shule ya bweni kwa ajili ya watoto yatima wakubwa na hapo ndipo patakuwa mahala pa kazi pa David baada ya ujenzi kukamilika. Ni wazi kwamba wazazi wake wanaunga mkono kwa dhati juhudi za David. Kuhusu marafiki zake je? Yeye hukutana nao kila Alhamisi katika jumba la starehe lijulikanalo kwa jina THE Place hapo mjini Arusha ambako wao hupendelea kusikiliza muziki wa bendi…..

18. **Atmo:** (Track 1010 file “Kloster” 0.41-0.50)

*(music and singing)*

19. **NARRATOR:**

…. Lakini mara tena watoto humjia David mawazoni mwake….

*20.* **OTONE David:** (Track 1033, English,0.18 – 0.38
Track 1034 Swahili)
*"Ninafarijika sana ninapowaona watoto hao wanatabasamu kila siku….ninahisi nimejawa na nguvu mpya hata sijali wanachokifanya rafiki zangu, wafanyakazi wenzangu au wanafunzi wenzangu chuoni."*

21. **NARRATOR:**
Sio kwamba hajali kile marafiki zake wanachokitegemea kutoka kwake. Ni kwamba anasikitishwa na watu ambao hawajitolei katika maswala ya jamii.

22. **OTONE David:** (Track 1033, English, 01.13 – 1.34
Track 1034 Swahili)
*"Nafikiri kwamba kuna watu wachache mjini Arusha au Tanzania nzima wanaojitolea kufanya jambo kwa ajili ya jamii zao. Watu wengi wanafanya bidii ya kutafuta mahitaji yao binafsi ya kila siku au chakula chao cha kila siku lakini yote hiyo haitoshi, lazima tuwe na moyo wa kusaidia jamii hasa kwa wale wanaohitaji msaada."*

23. **NARRATOR:**
Ni sawa. Marafiki na wafanyakazi wenzake wanaweza kusubiri lakini kinachomtia wasiwasi David ni mpenzi wake Marjori. Ana umri wa miaka 28 na walikutana mjini Nairobi wakati wakiwa masomoni.

24. **OTONE David:** (Track 1035 English, 0.03 - 0.32
Track 1036 Swahili)
"Ndio, nina mpenzi. Anashangazwa sana na mawazo yangu. Kwa upande mwingine ananiona kuwa mimi ni mtu mwenye ndoto ya ajabu na ninataka kufanikisha mambo mengi mazuri kiasi kwamba sitakuwa na muda wa kujumuika naye kama vile ningependa kuwa na muda kama huo kwa rafiki zangu wengine."

25. **NARRATOR**:
Kweli hayo ni mazito. Lakini hebu turudi kule kwenye makao ya watoto yatima na tuangalie ni kipi kinachompa moyo David katika kazi yake ya kila siku?

26. Atmo (13): (Track 1007, 0.02 - Children singing (in Swahili)
FADE INTO NARRATOR

27. **NARRATOR:**

Baadhi ya watoto hao wamepitia mambo mengi mazito katika maisha yao ya utotoni. Wamepigwa na wazazi wao au kutelekezwa na wengine hawakutakiwa kabisa na wazazi wao. Hakuna hata mmoja kati ya watoto wao anaeonekana kuwa ni mtoto yatima.. yaani wote wanaonekana ni watoto wa familia moja.

*28.* **O-Tone child (1)**: (Track 1022, English, 0.08 - 0.19
Track 1022, Swahili, 0.24 – 0.34)
”Napenda maji ya uzima. Kwa sababu wakati wote tunasoma na kucheza na mambo mengine*.”*

29. **NARRATOR**:

Na haya ni matunda ya kazi yake David.. na watoto wanampenda sana.

*30.* **O-Tone child (2):** (Track 1023, English 0.07 – 0.17
Track 1023, Swahili, 0.23 – 0.33)
”Anacheza mpira wa miguu na sisi na anatufundisha kusoma herufi*.”* **NARRATOR**:

Ni kweli makao hayo ya watoto ni mahala panapofaa maisha ya David, lakini pia kuna uwezekano wa kuwepo usumbufu,

usumbufu wenyewe ni kuhusu hasa jinsi ya kugundua chanzo cha matatizo.…

*34.* **O-Tone David**: (Track 1053, English, 0.22 – 1.00
Track 1054 Swahili)
”Kinacho nisumbua sana ni kutafuta chanzo cha tatizo. Inaanzia wapi mtoto alikotoka*. Hapo ndio kwenye tatizo kubwa. Inawezekana pia kuwa familia ya mtoto huyo ina uwezo. Lakini kukawa bado kuna tatizo –labda baba ana tabia ya kulala nje halafu baadae anamuambukiza mkewe UKIMWI . Hilo linanitatiza sana na kuniumiza moyo wangu kwa sababu hapo ndipo mtoto mwenye UKIMWI anapozaliwa.Shida iliyopo hapaTanzania ni kwamba jamii na marafiki inkuatenga na kukunyanyasa unapokuwa mtoto yatima aliyezaliwa kwenye hali hiyo ya ugonjwa wa UKIMWI. Hali hiyo inawatesa watoto kiakili na kimwili.”* **NARRATOR** Ndio maana ni muhimu kwa David kuwapa elimu nzuri. **Atmo: Children singing “Spelling-Rap” (Track 1073, Swahli)** 0.40 – 1.21 FADE INTO NARRATOR **NARRATOR**: Hatimae muhula wa mwaka umefika mwisho, kwa David hii ni nafasi ya mwisho ya kuweza kuwakumbusha wanafunzi juu ya majukumu yao. Hazingatii tu kuhusu umuhimu wa upendo na amani, nasaha yake iko wazi kabisa, kwamba bila juhudi hakuna mafanikio. **O-Tone David:** (Track 1074, English, 0.22 - 0.41 min
Track 1075, Swahili, remark of the author: please cut the

passage about “Friederike and Günter” and keep only the rest of the speech)

*”Mmefanya vizuri, muwe na wakati mwema, tutaonana hivi karibuni, tuna mambo mazuri siku ya Jumamosi na zinginezo zijazo na natumai nyote mtafurahia! Ok? Wakati mzuri!* **Atmo**: (Track 1075, 1.45 – 1.50) Clapping hands.

**OUTRO (Announcer):**

Hivyo ndivyo siku ya David na rafiki zake inavyomalizika. Ilikuwa pia ni siku ya mwisho wa mwaka wa shule, lakini sio mwisho wa makala ,bali mbali ya Noa Bongo jemga maisha Yako. Bado tuna mashujaa wengi watakao kutia moyo na kukupa muelekeo wa maisha, tutakutana na baadhi yao wakati ujao utakapo tusikiliza. Iwapo ungependa kumwambia rafiki yako au ungetaka kukisikiliza tena kipindi hiki, temebelea mtandao wetu na anuani yetu ni kama ifuatavyo: www.dw-world.de mkwaju lbe. Hadi wakati ujao Kwaheri.

**d w world dot de slash l b e (www.dw-world.de/lbe).**